

**MHE. SIMBACHAWENE ARIDHISHWA NA THAMANI YA FEDHA ILIYOTUMIKA  
KATIKA MRADI WA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA  
MWANANGWA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI**

Na. Veronica E. Mwafisi-Misungwi

Tarehe 05 Agosti, 2023.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amewapongeza Viongozi na Wananchi wa Kijiji cha Mwanangwa kwa kusimamia miradi mbalimbali kikamilifu baada ya kuridhishwa na thamani ya fedha iliyotumika katika mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mwanangwa iliyojengwa kupitia Mradi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) katika halmashauri ya Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

Mhe. Simbachawene ametoa pongezi hizo wakati alipokuwa akizungumza na walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na wananchi wa Kijijicha Mwanangwa, Kata ya Mabuki katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza wakati wa ziara yake ya kikazi katika halmashauri hiyo iliyolenga kukagua utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

“Nimefurahi sana na niwapongeze kwa kusimamia kikamilifu mradi huu wa TASAF wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wasichana Mwanangwa uliogharimu takribani milioni 168, mmenipitisha na kuukagua mradi huu kwa namna majengo yote haya yalivyojengwa kwa ufanisi mkubwa nimeridhika na thamani ya fedha ambayo imetumika hapa,” Mhe. Simbachawene amesema.

Aidha, Mhe. Simbachawene amewapongeza na kuwashukuru wananchi kwa kuchangia na kutumia nguvu zao pia katika kufanikisha ujenzi huo hali inayoonyesha jamii pia imeshiriki katika ujenzi wa Shule hiyo itakayowasaidia wanafunzi wa kike kuwa katika uangalizi mzuri na kuepuka vishawishi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Mhe. Paulo Chacha amemshukuru Waziri Simbachawene kwa kufanya ziara katika Wilaya ya Misungwi na kuahidi kuwa watumishi na wananchi wa Wilaya yake wataendelea kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano mkubwa ili kuleta maendeleo katika nchi.

Naye, Mbunge wa Jimbo la Misungwi, Mhe. Alexander Mnyeti amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu

Hassan kwa kuendelea kuwapatia fedha za miradi mbalimbali yakiwemo mabweni ya wanafunzi na vituo vya afya katika jimbo la Misungwi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amehitimisha ziara yake ya kikazi ya siku mbili katika mkoa wa Mwanza iliyolenga kukagua utekelezaji wa miradi ya TASAF pamoja na kuzungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na Misungwi mkoani Mwanza kwa lengo la kutatua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili watumishi wa halmashauri hizo.